

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA TISA**



12 APRILI, 2019

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA TISA – TAREHE 12 APRILI, 2019

I. DUA:

II. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**68. MHESHIMIWA SHAABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):**

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali imekuwa na utaratibu wa kukarabati Shule zake za Msingi na Sekondari nchini:-

Je, ni lini Serikali itazifanyia ukarabati Shule za Msingi za Kwemashai, Bandi, Milungui, Kilole na Shule za Sekondari za Ntambwe, Ngulwi – Mazashai na Mdando.

**69. MHESHIMIWA ZACHARIA PAUL ISSAAY  
(MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali ina nia njema ya kuuweka Mji Mkongwe wa Mbulu kwenye mpango kabambe wa maboresho ya Miji na Majiji, Mikoa na Wilaya; na kwenye Awamu ya Pili ya mpango huo kwa ajili ya miundombinu ya Masoko, barabara, Vituo vya mabasi na taa za barabarani:-

- (a) Kwa kuwa Mji huo ni Mji Mkongwe toka kuanzishwa kwake, Je, ni lini sasa nia hiyo njema itatekelezwa;
- (b) Je, mpango huo wa maboresho ya Mji utasaidiaje miundombinu ya barabara za Mitaa ya Mji wa Mbulu ambazo ni zaidi ya km 40 za changarawe kwa kuwa kuna km 1.8 za lami kwa sasa.

**70. MHESHIMIWA SAUL HENRY AMON  
(RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hakuna barabara ya kuunganisha Daraja la Nyubati na Kata ya Kisondolea hadi Nzunyuke umbali wa zadi ya Km 30 kufikia Kijiji cha Nyubati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya kuunganisha Kijiji cha Nyubati na Kata ya Kisondele.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**71. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Tabora – Mambali – Itobo – Kagongwa yenye urefu wa km 149 utanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwani ni ahadi ya Mhe. Rais na pia imo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 - 2020.

**WIZARA YA MAJI:**

**72. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIA BUKWIMBA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa Katoro – Buseresere unaokusudiwa kutoa maji Ziwa Victoria.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **73. MHESHIMIWA HAMIDU HASSAN BOBALI (MCHINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni cha muda mrefu na pia kimetumika kuandaa Viongozi wa nchi yetu na nchi jirani:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kukipandisha hadhi Chuo hicho kuwa Chuo Kikuu;
- (b) Je, kwa nini Serikali haipeleki fedha za maendeleo katika Chuo hicho kama zinavyopangwa.

### **74. MHESHIMIWA SUSAN PETER MASSELE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo Kikuu cha Umma au Vyuo Vikuu vya Umma vyenye hadhi ya juu katika Mkoa wa Mwanza.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **75. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Katika Jimbo la Mpwapwa Vijiji vya Mkanana, Nalamilo, Kiboriani, Igoji Kaskazini, Mbori, Tambi, Nana, Majani, (Mwenzele), Mafuto, Kiegea, Kazania, Chimaligo, Mbugani, Chihembe, Mazaza, Mwanjili, (Makutopa) na Chibwegele havina huduma ya umeme:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia huduma ya umeme Vijiji hivyo.

## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **76. MHESHIMIWA SIKUDHANI YASSIN CHIKAMBO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Idadi ya watu nchini inazidi kuongezeka sambamba na ongezeko la mahitaji ya ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea uwezo Wakulima na Wafugaji ili kuendeleza shughuli zao kwa tija zaidi na kuwaondolea adha wanazozipata.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **77. MHESHIMIWA FRANK GEORGE MWAKAJOKA (TUNDUMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itaunga mkono tamko la “Kilimo ndiyo Uti wa Mgongo wa Taifa kwa vitendo”.

### **III. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI) NA  
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA  
UTAWALA BORA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
12 APRILI, 2019**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**